

# HALMASHAURI YA WILAYA YA CHATO



Kumb. Na.CDC/05/20/91

Tarehe: 21/03/2018

## YAH: TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI.

Kufuatia Halmashauri ya wilaya ya Chato kupata kibali cha ajira **Kumb.Na.CFC.26/205/01"GG"/95 ya tarehe 12/03/2018** kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma kuhusu ajira mpya, MKurugenzi Mtendaji Wilaya ya Chato anatangaza nafasi za kazi na anakaribisha maombi kwa Watanzania wenye sifa za kujaza nafasi kama zilivyoorodheshwa katika tangazo hili:-

### **N.B MASHARTI YA JUMLA KWA KAZI ZOTE**

- i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri usiozidi miaka 45
- ii. **Waombaji wote waambatishe cheti cha kuzaliwa.**
- iii. Waombaji ambao tayari ni watumishi wa Umma na wamejipatia sifa za kuingilia katika kada tofauti na walizonazo, wapitishe barua zao za maombi ya nafasi za kazi kwa waajiri wao na Waajiri wajiridhishe ipasavyo.
- iv. Nafasi ya kazi inayoombwa iandikwe juu ya bahasha, kutozingatiwa hili kutasababisha maombi ya kazi kuwa batili.
- v. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika.
- vi. Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma, maelezo, nakala za vyeti vya kidato cha nne na kidato cha sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika. Viambatanisho hivyo vibanwe sawa sawa kuondoa uwezekano wa kudondoka au kupotea. Picha moja "Passport size" ya hivi karibuni iandikwe jina kwa nyuma.
- vii. Testimonials", "**Provisional Results**", "**Statement of results**", hati matokeo za kidato cha nne na sita (FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS)

### **HAVITAKUBALIWA.**

- viii. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (TCU na NECTA).
- ix. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wanakibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.
- x. Waombaji kazi ambao tayari ni waajiriwa katika nafasi za kuingilia walioko katika Utumishi wa umma wasiombe na wanatakiwa kuzingatia maelekezo yaliyo katika Waraka Na CAC. 45/257/01/D/140 wa tarehe 30 Novemba 2010.

xi. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kugushi wahusika watachukuliwa hatua kali za kisheria.

xii. Mwisho wa kupokea barua za maombi ni **tarehe 04 APRILI, 2018**

xiii. Maombi yanaweza kuandikwa kwa Lugha ya Kiswahili au Kiingereza na yatumwe kupitia posta ama moja kwa moja kupitia Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W) kwa anuani ifuatayo:-

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA CHATO**  
**SLP.116**  
**CHATO -GEITA**

**1. WATENDAJI WA VIJIJI DARAJA LA III - NAFASI KUMI NA NANE (18)**

**MAJUKUMU YA KAZI**

- Afisa masuhuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji
- Kusimamia ulinzi na usalama wa raia na mali zao,kuwa mlinzi wa amani na msimamizi wa utawala bora katika kijiji.
- Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa Mipango ya Mendeleo ya kijiji.
- Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya kijiji
- Kutafsiri na kusimamia sera,sheria na taratibu
- Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa,umasikini na kuongeza uzalishaji mali.
- Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya Kitaalam katika kijiji
- Kusimamia,kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za kijiji.
- Mwenyekiti wa kikao cha wataalaamu waliopo katika kijiji
- Kupokea kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya wananchi.
- Kusimamia utungaji wa sheria ndogo za kijiji na
- Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata.

**SIFA ZA MWOMBAJI**

- Kuajiriwa mwenye elimu ya Kidato cha nne/sita aliyehitimu mafunzo ya Astashahada/Cheti Katika moja wapo ya fani zifuatazo: **Utawala,Sheria,Elimu ya Jamii, Msaidizi wa fedha,Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya sanaa** kutoka chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo,Dodoma au chuo chochote kinachotambuliwa na serikali.

**MSAHARA**

- Kwa kuzingatia ngazi za mishahara ya Serikali yaani **TGS B** kwa mwezi.

Imetolewa na;

Eng.Joel B.Hari

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**

**CHATO.**

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**

**S. L. P. 116**

**CHATO**